

HADITHI FUPI KUHUSU MAISHA YA BOB MARLEY

A short story about life of Bob Marley

Imeandikwa na Andy Meyers

Bob Marley alizaliwa tarehe sita mwezi wa pili mwaka elfu moja mia tisa na arobaini na tano katika kijiji kidogo kinachoitwa Nine Miles katika Parokia ya Mtakatifu Ann huko Jamaica. Jina lake kamili ni Robert Nesta Marley. Baba yake ni Mzungu aliyeitwa Noval Siclair Marley na Mama yake ni Mjamaika aliyeitwa Cadella ‘Ciddy’ Malcom.

Bob Marley alipofika umri wa miaka saba alichukuliwa na mama yake kuhamia Trenchtown ambako waliishi katika mageto. Huko aliaanza kupenda muziki hasa kwa vile akisikia miziki ya watu kama Ray Charles. Katika mwaka elfumoja mia tisa na sitini na moja, Bob Marley alikuwa umri wa miaka kuminasita (16) na alitaka kuanza kurekodi muziki. Katika mwaka elfu moja mia tisa na sabini na tano Bob Marley na wenzake walianzisha kikundi cha Muziki kilichojulikana kama “Wailers”. Mwaka elfu moja mia tisa na sitini na nane alisafiri kwenda Sweden kurikodi muziki na Johnny Nash. Alirekodi nyimbo kama “Stir it up” na nyenginezo.

Kuanzia mwaka elfu moja mia tisa na sabini na tano alipendwa sana huku Marekani na Uingereza. Na mwaka elfu moja mia tisa na sabini na sita mtindo wa Rege ulikuwa maarufu sana dunia nzima. Katika Jamaica, Bob alianza kujulikana na mtume na baadhi ya watu wa Jamaica waumini wa dhehebu la KiRastafari.

Katika mwaka elfumoja mia tisa na sabini na nane Onyesho kubwa lililoitwa “One Love”(Pendo Moja) ambalo liliandaliwa kwa ajili ya kuwakutanisha Rais Michael Manley na Kiongozi wa Chama cha Upinzani, Bwana Edward Siaka ili kuleta amani katika Jamaica. Bob baadaye alipokea Nishani ya Amani kwa nchi za Dunia ya Tatu ya Umoja wa Mataifa huko New York. Bob pia alitembelea nchi nyingi zikiwemo za Kiafrika kama Kenya, Zimbabwe na Ethiopia. Huko Zimbabwe alikwenda kwa ajili ya sherehe za uhuru wa nchi hiyo.

Tarehe kuminamoja, mwezi wa mei mwaka wa elfu moja mia tisa na thamanini na moja Bob Marley alifariki dunia baada ya kuumwa na maradhi ya Kansa iliyoanza na kidole gumba.. Bob alizikwa kijijini kwao cha Nine Miles huko Jamaica na maziko yake yalihudhuriwa na mamia na maelfu ya watu wa Jamaica. Bob Marley alikuwa kiongozi katika jamii ya Jamaica na dunia kwa sababu ya nyimbo zake zenye wito wa amani na umoja wa Waafrika. Yeye ni mmoja ya wanamuziki wenye atayekumbukwa wakati wote.